



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

UTOAJI WA LESENI ZA MUDA MFUPI KIPINDI CHA MWISHO WA MWAKA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawataarifu wamiliki wa magari ya abiria kuwasilisha maombi ya leseni za muda mfupi (short term licence) kwa ajili ya kutoa huduma kwenye njia ambazo huwa na uhitaji mkubwa wa huduma za usafiri wa abiria kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Leseni hizo zitatolewa kuanzia tarehe 08 Desemba, 2022 kwa magari ya abiria yanayokidhi vigezo vifuatavyo;

- i) Uwezo wa kubeba abiria arobaini (40) au zaidi,
- ii) Kufungwa kifaa cha kufuatilia mwenendo wa gari (VTS)
- iii) Kuwa na Bima iliyo hai
- iv) Kuunganishwa kwenye mfumo wa tiketi mtandao (e-ticketing)
- v) Kukaguliwa na Wakaguzi wa Magari wa Jeshi la Polisi au Kituo cha Ukaguzi wa Magari kilichopo katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), ili kubaini kama linafaa kwa matumizi ya safari,
- vi) Liwe na leseni hai ya LATRA.

Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa utoaji leseni ujulikanao kama <https://rrims.latra.go.tz> na kuambatanisha nyaraka zifuatazo;

- i) Nakala ya Kadi ya gari,
- ii) Nakala ya Hati ya Bima,
- iii) Nakala ya Ukaguzi wa gari kutoka Jeshi la Polisi au NIT
- iv) Uthibitisho wa utoaji tiketi mtandao na jina la mtoa huduma (vendor) wa tiketi Mtandao.

Maombi yanaweza kutumwa muda wowote kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia simu namba **0800110019** au barua pepe info@latra.go.tz au fika ofisi za LATRA zilizopo mikoa yote Tanzania Bara.

Imetolewa na:
Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano
24 Novemba, 2022